

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA IGUNGA

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

SHULE YA SEKONDARI ZIBA

S.L.P 12

IGUNGA-TABORA

TAREHE.....

Kumb Na ZSS/JI/.....

MWANAFUNZI

SHULE YA MSINGI.....

S.L.P.....

IGUNGA.

YAH : MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZIBA KIDATO CHA MWAKA

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga katika shule ya sekondari Ziba iliyopo wilayani Igunga , Mkoa wa Tabora , Shule ipo km 27 kutoka Nzega na km 58 kutoka Igunga.

Aidha ni matumaini yetu kuwa utaendeleza ari ya kusoma kwa bidii uwapo shuleni utatakiwa kusoma, kufanya kazi za nje kwa bidii na kutii sheria za shule , kuheshimu viongozi wa ngazi zote na kuonyesha heshima kwa jamii inayokuzunguka wakati wote.

Shule itafunguliwa tarehe hivyo unapokuja shuleni ni muhimu kuja na mahitaji yote kama fomu hii inavyoeleza .

KARIBU SANA ZIBA-MASTERY FOR SERVICE

Nakutakia maandalizi mema

.....

ALLY .M.NOHOYE

MKUU WA SHULE

0754411332

KIAMBATISHO NO 1

SARE ZA SHULE

(A) WASICHANA

- Sketi mbili nyeusi kitambaa kizito chenye marinda 14 yasiyozidi inch 1.5 ya kuelekea upande mmoja na urefu wake ufunike magoti.
- Mashati mawili tetron mikono mifupi pamoja na soksi nyeupe ndefu
- Viatu vyeusi vyenye kamba vya ngozi visivyo na urembo wala isigino virefu na soksi ndefu nyeupe

- Wasichana wa *Kiislamu wanaopenda kuvaa Hijab wakati wa masomo wanaruhusiwa* lakini hijab iwe ya kushona nyeupe isiwe ya dukani, Nusu kanzu nyeupe isiyobana na sketi ndefu yenye linda box moja mbele na moja nyuma.

(B) WAVULANA

- Mashati mawili meupe (tetron) mikono mifupi
- Suruari mbili zisizo na zaidi ya marinda mawili, mifuko miwili ya pembeni na mmoja wa nyuma.
- Viatu vyeusi vyenye kamba vya ngozi pamoja na soksi nyeusi.

NB: Mshono wa modal haurusiwi

VIFAA VYA DARASANI

- ❖ Madaftari makubwa 12 ya kuandikia masomo darasani
- ❖ Madaftari makubwa 12 ya majaribio
- ❖ Mkebe wa vifaa vya hesabu/Mathematical set (bofa)
- ❖ Kalamu na penseli bila kusahau Rula

VIFAA VYA MICHEZO

Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vya michezo kama raba , bukta ,tracksuit, socks na Tshirt aina ya jezi

KIAMBATISHO NO 2

SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya 1978 ambayao ilifanyiwa marekebisha 1995 ambapo uwapo shuleni unapaswa;

- ❖ Kuheshimu viongozi wa siasa, serikali , wazazi , walimu , watumishi , wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla
- ❖ Kuhudhuria na kuwahi kila siku shuleni bila kukosa
- ❖ Kujua na kuelewa mipaka ya shule
- ❖ Kuwa msafi wakati wote
- ❖ Kuwahi katikashughuli zote za shule na nyingine unazopangiwa

KIAMBATISHO NO 3

AJE NA VIFAA VYA KUFANYIA USAFI NA SHUGULI ZA NJE

- ✓ Ufagio wa nje, ndoo moja ya lita kumi na jembe moja

WANAFUNZI WA HOSTEL

Huduma ya Hosteli ni hiyari kwa hiyo kuna fomu maalumu zinazopatikana shuleni ofisi ya Mkuu wa Shule.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
MKUU WA SHULE